

MAVAZI YA WANAWAKE WA KIISLAMU

NAMNA GANI MWANAMKE AVAE ANAPOKUWA

PAMOJA NA WANAWAKE WENZAKE ?

(2)

(1)

وأما المرأة مع المرأة المسلمة - طبعًا - فهي عورة، إلا مواطنَ الزينة منها، وهي: الرأس، والأذن، والتحرُّ، وأعلى الصدر - موضع القلادة - والدرع، مع شيءٍ من العُضد - موضع الدُمْلج - والقدم، وأسفل الساق - موضع الخلخال - وما سوى ذلك فعورة لا يجوز للمرأة - كالمحارم - أن تنظرَ إلى شيءٍ منها، ولا أن تُبديَه؛ لصريح قوله تعالى: وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَى جُوهِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ أَوْ نِسَائِهِنَّ). (تلاخيص أحكام الجنائز) (ص:30).

Amesema Imaamul Albaaniy ALLAH amrehemu;

“ Ama mwanamke anapokuwa pamoja na mwanamke mwenzake - ndiyo - bado (mwili wake) utakuwa ni uchi isipokuwa maeneo ya mapambo yake nayo ni; **kichwa , na masikio, na shingo na juu ya kifua chake (karibu na shingo) sehemu ya (kuteremkia) kidani cha shingoni , na dhira za mkono wake pamoja na sehemu fulani ya kifupa panya yaani sehemu ya bangili ya juu ya mkono (karibu na bega), na miguu na chini ya muundi- ambayo ni sehemu ya bangili za miguuni (vikuku). Na viungo tofauti na hivyo ni uchi, haifai kwa mwanamke kutazama viungo hivyo (kwa mwanamke mwenzake) wala pia haifai kuviacha wazi kama vile mwanaume wa kando asivyofaa kutazama**

chochote katika viungo hivyo. Kwa sababu ya uwazi wa kauli ya AL-LAH aliposema ((... na wala wanawake wasidhihirishe mapambo yao **isipokuwa** kwa waume zao au baba zao au baba wa waume zao au watoto wao wa kiume au watoto wa kiume wa waume zao au kaka zao au watoto wa kiume wa kaka zao au watoto wa kiume wa dada zao **au wanawake wenzao** ..))

فتاوى اللجنة الدائمة - 1 (288 / 17)

على المرأة أن تحتشم وتتحملى بالحياء، حتى ولو لم ينظر إليها إلا نساء، ولا تكشف لهن إلا ما جرت العادة بكشفه ودعت له الحاجة، كالخروج لهن في ثياب البدلة، مكشوفة الوجه واليدين وأطراف القدمين ونحو ذلك، وذلك أستر لها وأبعد عن مواطن الريبة

Wamesema wanachuoni wa jopo la fat'wa na tafiti za kielimu la Saudi Arabia:

“ Ni wajibu juu ya mwanamke wa kiislamu ajiheshimu na ajipambe na aibu (haya), hata kama hakuna anayemtazama isipokuwa mwanamke mwenzake, na wala asifunue kiungo chochote (mbele yao) **isipokuwa kile ambacho ni kawaida kudhihirika kwake na kuwe na haja (sababu ya msingi) ya ufunuaji huo; kama vile kufunua uso na mikono miwili na ncha za miguu miwili (karibu na nyayo) na mfano wa viungo hivyo;** na kufanya hivyo ni jambo lenye kumsitiri zaidi mwanamke na kumuweka mbali zaidi na maeneo ya fitina...”

Mwisho: